

MWENGE WA UHURU WARIDHISHWA NA MAENDELEO YA UTEKELEZAJI WA MRADI MKUBWA WA MAJI JIJINI ARUSHA.

Mwenge wa Uhuru umetembelea na kukagua utekelezaji wa mradi Mkubwa wa Maji Jijini Arusha ikiwa ni pamoja na kuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo unaofadhiliwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mhe. Rais Dkt John Pombe Joseph Magufuli.



Ukiwa katika mbio zake mwaka huu Jijini Arusha, Mwenge wa Uhuru umetembelea na kukagua maendeleo ya miradi miwili ya maji inayosimamiwa na AUWSA ya kisima cha maji cha Oloirien, na ujenzi wa tenki la maji lenye uwezo wa kupokea maji kiasi cha lita milioni 3. Mradi wa uchimbaji wa kisima cha Oloirien umegharimu takribani Shilingi milioni 84.6 na una uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha lita 8,000 kwa saa sawa na lita 192,000 kwa siku.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa tenki katika eneo la mlima Burka Kata ya Olasiti kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2019, Mkurugenzi wa AUWSA Eng. Ruth S. Koya amesema kuwa mradi huo ni sehemu ndogo tu ya mradi mzima kwani mradi wenyewe umegawanywa katika vipengele vitatu ili kurahisisha utekelezaji wake ambavyo ni Uboreshaji wa huduma ya usambazaji wa Majisafi na miundombinu yake, Uboreshaji wa huduma ya Usafi wa Mazingira na miundombinu yake na Kujenga uwezo wa taasisi.

Mkurugenzi Koya akasema kuwa Mradi wa ujenzi wa tenki katika eneo la mlima Burka ni sehemu ndogo tu ya mradi mzima kwani mradi wote kwa jumla unagharimu zaidi ya shilingi 520 bilioni huku huu wa ujenzi wa tenki ukigharimu 2.3 Bilioni pekee.

Eng. Koya amedokeza kuwa mradi huu utapokea maji kiasi cha lita milioni 3 kutoka katika tenki lingine kubwa lililopo Ngaramtoni ambalo nalo litakuwa likipokea maji hayo kutoka katika visima vya Shamba la Mbegu vilivyopo eneo la Kimnyaki na Olmringaringa Wilayani Arumeru.

Mhandisi Koya amesema wanufaika wa mradi husika ni wakaazi wa Kata za Olasiti, Sombetini, Osunyai, Sokon I, Murieti, na Terrati wapatao 156,320. "Pamoja na tenki hili pia AUWSA imepanga kujenga matenki mengine 11 katika maeneo mengine likiwemo lile la Ngorbob, Olmoti, Mlima CCM, Themis, Moshono, Moivo, na mengineyo".

Akieleza manufaa ya mradi huo Mhandisi Koya amebainisha kuwa Uzalishaji wa maji utaongezeka toka wastani wa lita 40,000,000 hadi lita 200,000,000 kwa siku. Mradi utaongeza idadi ya wakazi wanaopata maji toka wastani wa watu 325,000 hadi kufikia watu 600,000 wakiwemo wastani wa watu 250,000 wanaoingia na kutoka Jijini kila siku.

Mkurugenzi pia amemwambia kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kuwa mradi kwa ujumla wake utapunguza maji yanayopotea toka wastani wa 40% hadi 25% na kuongeza mtandao wa bomba za majisafi toka 44% hadi 100%.

Kwa upande wa majitaka Mkurugenzi Koya amesema mradi utaongeza mtandao wa kukusanya majitaka kutoka 7.66% hadi 30% na kujenga mabwawa mapya ya kutibu majitaka ikiwa ni pamoja na kupunguza kero ya uzibaji wa mabomba ya majitaka.

Mwenge wa Uhuru Mwaka huu umebeba ujumbe "MAJI NI HAKI YA KILA MTU, TUTUNZE VYANZO VYAKE NA TUKUMBUKE KUSHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA"

MWISHO
